TANGAZO LA SERIKALI Na. 241 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 9025 la 2023

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ya Mwaka 2023 ambayo hapa imerejewa kama “Sheria Ndogo Kuu”.

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

**2**. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza kwa-

(a) kufuta vipengele (c), (d) na (e) vya Sehemu ya Pili na kuviandika upya kama ifuatavyo:

“SEHEMU YA PILI
USHURU WA MAEGESHO NA USHURU WA KUVUKA MPAKA

| Na. | Aina ya gari | Kiasi cha ushuru (kwa siku) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa kuvuka na kuvusha bidhaa mpaka wa Horohoro: | |
| | (c) Tandam | 15,000/= |
| | (d) Semi trela | 20,000/= |
| | (e) Lori lenye tela | 30,000/= |

(b) kufuta vipengele (a) na (f) vya Sehemu ya Nne na kuviandika upya kama ifuatavyo:

"SEHEMU YA NNE
USHURU WA MAZAO YA UVUVI

| Na. | Maelezo | Kiwango kwa siku |
|---|---|---|
| 2. | (a) Samaki wabichi | Shilingi 3,00/= kwa kila ndoo kubwa |
| | | Shilingi 1,500/= kwa kila ndoo ndogo |
| | (f) Dagaa wakavu | Shilingi 100/= kwa kila kilo 1 |

Dodoma
12 Machi, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi- OR-TAMISEMI*